

BODI YA MIKOPO YA ELIMU YA JUU ZANZIBAR (BMEJZ) INAWAJULISHA WAOMBAJI WOTE KUWA IMESHATANGAZA AWAMU YA KWANZA YA MAJINA YA WAOMBAJI 1,021 WALIOTEULIWA KUPATA MIKOPO YA ELIMU YA JUU KATIKA MWAKA WA MASOMO 2017/18.

MAJINA HAYO YAMEWEKWA KATIKA TOVUTI NA FACEBOOK YA WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI ZANZIBAR. AIDHA, MAJINA HAYO YATATANGAZWA KATIKA GAZETI LA ZANZIBAR LEO LA TAREHE 27/10/2017.

KWA WAOMBAJI WOTE WATAKAOYAONA MAJINA YAO KATIKA ORODHA ZA WAOMBAJI WATAKAOPATIWA MIKOPO WANATAKIWA KUZINGATIA YAFUATAYO:

1. KILA MWOMBAJI LAZIMA AJAZE MKATABA WA MIKOPO UNAOPATIKANA KATIKA OFISI ZA BMEJZ. WANAFUNZI WANAOSOMA KATIKA VYUO VILIVYOPO TANZANIA BARA NA NJE YA NCHI WATAKIWA KUFIKA KWENYE OFISI ZA BMEJZ KUANZIA SIKU YA IJUMAA TAREHE 27/10/2017. OFISI ZITAKUWA WAZI SIKU YA JUMAMOSI TAREHE 28/1-/2017 ILI KUENDELEA KUTOA HUDUMA ZA UTOAJI MIKATABA YA MIKOPO. HAKUNA MWANAFUNZI ATAKAYEFANYIWA MALIPO YA MIKOPO BILA YA KUJAZA MKATABA WA MIKOPO.
2. MWOMBAJI ALIYEPATA MIKOPO KUTOKA BODI YA MIKOPO YA WANAFUNZI WA ELIMU YA JUU TANZANIA (HESLB) JINA LAKE LITAONDOSHA KATIKA ORODHA YA WAOMBAJI WALIOPATIWA MIKOPO NA BMEJZ.
3. MIKOPO INAYOTOLEWA NA BMEJZ HAIWAHUSU WAAJIRIWA WA TAASISI ZA SERIKALI.